ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
6.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
7.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
9.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
15.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
16.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
20.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
21.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
23. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.

24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
25.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
27.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
28.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
29.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
32.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.
33.Mhe. Hamad Masoud Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
34.Mhe. Omar Ali Shehe	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.

35.Mhe. Rashid Seif Suleiman	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
36.Mhe. Mohamed Ali Salim	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
37.Mhe. Asaa Othman Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
38.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
39.Mhe. Najma Khalfan Juma	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
41. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
44.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
45.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
46.Mhe. Ali Moh'd Bakari	Jimbo la Tumbe.
47.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
48.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
59.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.

50.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
51.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
52. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
53.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
54.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
56.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
57.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
58.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
59.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
60.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
61.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
62.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
63.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
64.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
65.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
66.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
67.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
68.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
69.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.

70.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
71.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
72.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
74.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
75.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
76.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Nafasi za Wanawake.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 30 Oktoba, 2009

(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)

Dua

Mhe. Spika (Mhe. Pandu Ameir Kificho) Alisoma Dua

KUAHIRISHWA BARAZA

Mhe. Waziri Kiongozi: Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu mwenye rehema, kwa kutuwezesha kutekeleza kwa ufanisi shughuli za Baraza lako tukufu. Pili, nakushukuru wewe Mhe. Spika kwa kuuendesha vyema mkutano huu kwa hekima na busara kubwa. Tatu, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwa kuuliza maswali mazuri kuhusu utendaji wa shughuli za Serikali na kuishauri ipasavyo wakati wa kujadili hoja zilizowasilishwa hapa Barazani. Mwisho, nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri kwa kuyajibu vizuri maswali yalioulizwa pamoja na kutoa ufafanuzi wa hoja mbali mbali.

Katika mkutano huu jumla ya maswali 72 ya msingi yaliulizwa na kujibiwa na Waheshimiwa Mawaziri. Vile vile, Baraza lilijadili na kuipitisha miswada sita ya sheria kama ifuatayo:-

1. Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Kukuza Utalii namba 9 ya 1996 na Kutunga Sheria ya Utalii ya 2009.
2. Mswada wa sheria ya Masharti ya Usimamizi wa Sheria za Kodi.
3. Mswada wa sheria wa Kurekebisha Sheria ya Bodi ya Mapato Nam. 7 ya 1996.
4. Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Madawa ya Kulevya na kuzuiya usafirishaji haramu wa madawa ya kulevya na kuweka masharti ya uzuiaji, usafirishaji haramu wa madawa ya kulevya.
5. Mswada wa Sheria ya Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu.
6. Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar namba 8 ya 1999.

Mhe. Spika, Baraza lako tukufu lilipitisha mswada wa sheria ya kufuta sheria ya Kukuza Utalii Nam. 9 ya 1996 na kutunga sheria ya utalii ya 2009 kwa lengo la kuondoa kasoro zilizojitokeza katika kukuza biashara ya utalii. Kasoro hizi ni udhaifu wa utoaji wa taarifa za utalii, usalama mdogo wa watalii na muundo dhaifu wa Kamisheni ya utalii.

Mhe. Spika, Sheria hii mpya inarekebisha kasoro hizo tatu nilizozitaja hapo awali. Kwanza, sheria itaimarisha upatikanaji wa taarifa sahihi kuhusu idadi ya hoteli na wageni wanaofika kwenye hoteli hizo. Jambo hili litasaidia kupunguza na kudhibiti vitendo vya udanganyifu katika kulipa kodi za utalii na hivyo kuiwezesha Serikali kupata mapato stahiki kwa kugharamia mipango ya maendeleo.

Pili, sheria inawawekea utaratibu maafisa wa utalii kutembelea mara kwa mara maeneo ya utalii ili kuzuia uhalifu dhidi ya watalii. Ili kudumisha usalama wa watalii wananchi nao wana mchango mkubwa katika kuwapatia askari wa Jeshi la Polisi na maafisa wa utalii taarifa za uhalifu kwa wakati mwafaka. Tatu, sheria hii inaufanyia marekebisho muundo wa Kamisheni ya utalii ili kuunda Bodi ya Wakurugenzi. Marekebisho haya yanatarajiwa kuiongezea Kamisheni ya Utalii ufanisi katika kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Spika, kama tunavyojua sekta ya Utalii ina mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa Zanzibar. Ili kufikia lengo hili serikali ina wajibu wa kuimarisha miundombinu na kuongeza vivutio vya utalii. Kwa upande mwengine wawekezaji wa sekta ya utalii nao wanatakiwa waongeze ubora wa huduma wanazozitoa ili hoteli zao ziweze kukidhi mahitaji ya wateja wao.

Kwa mfano, hoteli nyingi ziliopo Zanzibar hivi sasa zinatoa huduma za utalii wa daraja wa chini na kati. Ipo haja ya kuwavutia watalii wa daraja la juu ili kuiongezea serikali mapato makubwa.

Mhe. Spika, katika kufikia lengo hili wananchi na wafanyakazi wa sekta hii wapatiwe elimu na mafunzo ya kutosha katika Chuo cha Maendeleo ya Utalii na Vyuo vingine ili waweze kuongeza ujuzi wao katika utoaji wa huduma bora za utalii. Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na Chuo Kikuu cha Zanzibar wanashauriwa waanzishe vitivo vya elimu ya utalii na uongozi ili kuongeza idadi ya wataalamu wa sekta ya utalii hapa Zanzibar. Suala hili litawasaidia vijana wa Zanzibar kuajiriwa katika nafasi za uongozi wa hoteli za kitalii kinyume na ilivyo sasa.

Mhe. Spika, juhudi za kuimarisha biashara ya utalii zinatakiwa ziende sambamba na uimarishaji wa vivutio vya utalii tulivyonavyo sasa. Itakuwa jambo la kufurahisha iwapo wawekezaji wa sekta hiyo ya utalii wataanzisha ziara za kutembelea maeneo ya utalii katika Mji Mkongwe kwa kutumia magari ya wazi kama wanavyofanya wenzetu nchi za nje. Mji kama Dubai na London wanazo huduma za kuwatembeza wageni kwa kutumia mabasi maalum. Vile vile tunazo fursa kubwa za kuanzisha huduma za kuwasafirisha watalii kwa maboti kutembelea maeneo mbali mbali hasa kwenye visiwa vidogo ili waone mandhari mwanana ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kutokana na udhaifu wa kuvitangaza vivutio vya utalii vya Zanzibar, idadi ya wageni tunayopata bado ni ndogo sana ikilinganishwa na nchi kama Mauritius na Syschelles wakati nchi zote hizi hazina vivutio vingi na vizuri kama tulivyonavyo sisi Zanzibar. Kwa hivyo, kuna haja ya kuitangaza Zanzibar Kimataifa hasa kwa kutumia Ofisi za Kibalozi nje ya nchi, vyombo mbali mbali vya habari vya Kimataifa kama *CNN*, *Travel* Ch*a*nnels na *Discovery* Channels na kutumia "*Internet*" katika kuutangaza utalii wa Zanzibar. Hapana shaka tukizichukua hatua hizi idadi ya wageni wanaoitembelea Zanzibar itaongezeka kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi imeamua kuanzisha biashara ya utalii ili kutoa fursa za ajira, kuongeza mapato na kuimarisha soko la mazao ya kilimo, uvuvi na ufugaji. Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira ina wajibu wa kuweka mipango madhubuti kuimarisha kilimo ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya vyakula, matunda, viungo, mboga mboga, kuku, mayai na samaki. Inasikitisha sana ninaposikia baadhi ya wananchi wa Zanzibar wanakosa soko la mazao yao katika hoteli za kitalii.

Mhe. Spika, ili wananchi waweze kupata soko la mazao yao katika hoteli za kitalii hawana budi kuanzisha mashamba ya kilimo na ufugaji ya kibiashara ili wazalishe mazao kwa wingi na ubora wa hali ya juu. Mpango huu wa Kilimo umeweza kuzisaidia nchi nyingi kukuza Utalii na Kilimo na hatimaye kuwapatia wakulima vipato vikubwa. Kwa hiyo, utaratibu huu pia utawasaidia wakulima wa Zanzibar kupunguza matatizo ya umaskini.

Mhe. Spika, Mji Mkongwe wa Zanzibar ambao umeteuliwa kuwa moja ya hifadhi ya urithi wa Kimataifa Duniani ni kivutio kikubwa kwa watalii wanaotembelea Zanzibar. Baraza la Manispaa lina wajibu mkubwa wa kuutunza na kuuweka katika hali ya usafi ili kukuza haiba ya nchi yetu. Nimefarajika sana na hatua ziliochukuliwa hivi karibuni na Mkurugenzi mpya za kuzifufua taa za mitaani katika Mji Mkongwe. Hili ni jambo la kufurahisha sana na kutia moyo. Hatua hii inaweza kusaidia sana katika kupunguza vitendo vya uhalifu katika vichochoro mbali mbali vya Mji Mkongwe. Kwa hivyo, naomba Baraza la Manispaa chini ya Mkurugenzi mpya, kulisimamia jambo hili, lisiwe ni la kupita tu, bali liwe ni jambo la kudumu.

Mhe. Spika, vile vile Baraza la Manispaa linatakiwa kutengeneza bustani za kupumzikia wageni na wananchi. Kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu, hivi sasa bustani ya Forodhani haitoshi tena. Naliomba Baraza la Manispaa na Halmashauri za Wilaya zote kuangalia uwezekano wa kuanzisha bustani maalum za kupumzikia watu katika maeneo mbali mbali kama ile ya Forodhani, ili kuwasaidia wananchi kupata huduma hii muhimu katika maeneo yao.

Halikadhalika, mamlaka hizi ziandae utaratibu wa kupanda miti ya kivuli ili kuufanya mji wetu uwe wa kupendeza kama ilivyo miji ya wenzetu.

Mhe. Spika, pamoja na juhudi mbali mbali tunazozichukua katika kukuza utalii, kumekuwepo na vitendo vya uchafuzi wa mazingira hasa katika maeneo ya utalii. Baadhi ya mahoteli yanatupa taka ovyo wakati sheria inawataka wawe na mitambo maalum ya kuchomea takataka katika hoteli zao. Vile vile wapo baadhi ya wawekezaji wanaojenga kwenye fukwe kinyume na taratibu za ujenzi. Hali hii inasababisha uharibifu mkubwa sana wa mazingira katika fukwe kwa ujumla.

Mhe. Spika, upo uhusiano mkubwa kati ya uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya hali ya hewa duniani. Hivi sasa dunia inakabiliwa na tatizo kubwa la mabadiliko ya hali ya hewa. Mabadiliko ya hali ya hewa yanayotokea yanasababishwa na uchafuzi wa mazingira. Uchafuzi huu wa mazingira unajumuisha ukataji miti ovyo na ongezeko la kiwango cha gesi inayosababisha joto hasa kutoka viwandani.

Mhe. Spika, kwa ujumla kuongezeka kwa hali ya joto duniani kunasababisha mambo yafuatayo:-

1. Kubadilika kwa misimu ya mvua.
2. Kuongezeka kwa kina cha maji Bahari.
3. Kutokea kwa mafuriko.
4. Kutokea kwa Mmong'onyoko wa fukwe.
5. Kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo.
6. Kupungua kwa misitu.
7. Kuzuka kwa magonjwa ya joto katika sehemu za baridi kama vile malaria.
8. Kuyeyuka kwa barafu katika milima na pembezoni mwa Dunia.

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema hapo awali, mabadililo ya hali ya hewa duniani yana athari kubwa sana kwa maisha yetu. Athari hizi zimeshaanza kujitokeza hapa Zanzibar. Kama mnavyojua miongo ya mvua tayari imeshaanza kubadilika ama kwa kukosekana kabisa mvua au kwa kunyesha kwa kiwango kidogo sana. Kwa upande wa Zanzibar mabadiliko haya kwa ujumla wake yana athari sita zifuatazo:-

1. Kuongezeka kwa kasi ya mmong'onyoko wa fukwe.
2. Kupotea kwa baadhi ya visiwa vigodo katika sehemu mbali mbali za bahari ya Zanzibar.
3. Kutotabirika kwa mvua za masika na vuli kunakosababisha uzalishaji mdogo wa mazao ya kilimo.

4. Kuongezeka kwa joto. Taarifa za wataalamu zinaonyesha joto limeongezeka kwa zaidi ya sentigredi 1.
5 Kina cha bahari kikiongezeka kidogo Zanzibar maeneo ya Pongwe na Matemwe huenda yakafunikwa na bahari.
6. Wanasayansi wametabiri kuwa visiwa vya Zanzibar huenda vikatoweka baada ya miaka 100 kama kasi ya uharibifu wa mazingira inayoendelea sasa itaongezeka kwa kasi.

Mhe. Spika, ili tuweze kukabiliana na hali hii tunapaswa kuchukua hatua zifuatazo, ili haya niliyoyaeleza yasitokee Zanzibar.

1. Kuongeza kasi ya upandaji miti hasa katika maeneo ya wazi yaliyoharibika. Miti inasaidia kufyonza gesi inayosababisha joto kutoka viwandani.
2. Kutumia nishati ya jua, upepo na gesi.
3. Kupunguza uingizaji wa mafriji na magari mabovu.
4. Kupunguza uchimbaji mawe na mchanga hasa karibu na fukwe.

Tukizichukua hatua hizi basi zile athari nilizozieleza awali tunaweza kuzidhibiti kwa kiasi kikubwa sana Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Spika, katika mwezi wa Disemba, mwaka huu wa 2009 nchi mbali mbali duniani zinatarajiwa kuhudhuria mkutano maalum wa mazingira huko Copenhagen Denmark, kwa lengo la kuzishauri nchi zenye viwanda vingi duniani, kupunguza gesi zinazosababisha uharibifu wa mazingira. Ni vigumu sana kutabiri kile kitakachotokea katika mkutano huo muhimu, ila nchi zinazoendelea hazitarajii miujiza katika mkutano huo. Nchi nyingi zilizoendelea zinaamini, kuwa si rahisi sana kuzishawishi nchi zenye viwanda vikubwa duniani, kupunguza uzalishaji wa gesi joto, kwa sababu wanaamini hatua hiyo itasaidia sana kukuza chumi zao.

Mhe. Spika, yamekuwepo majadiliano pia ya kuzitaka nchi zinazoanza kukua kiuchumi kama India na China nazo zichukuwe hatua madhubuti ya kupunguza uzalishaji wa gesi joto katika viwanda. Jambo ambalo si rahisi sana kufikia hatua hiyo. Ndio maana nimesema hapo awali, katika mkutano huo pengine kutakuwa na mjadala mkubwa sana juu ya hatua hizo.

Mhe. Spika, mswada wa pili uliojadiliwa katika Baraza lako tukufu ulikuwa ni Mswada wa Sheria ya Masharti ya Usimamizi wa Sheria za Kodi. Madhumuni ya mswada huu ni kurahisisha usajili wa walipa kodi wanaosajiliwa na Bodi ya

mapato, ili kuhakiki na kuufuatilia pale itakapotokea walipa kodi hao wameshindwa kutekeleza wajibu wao. Utaratibu huu mpya hauna lengo la kuwasumbua walipa kodi, bali unakusudia kuhakikisha kwamba kila mlipa kodi anatekeleza wajibu wake wa msingi katika kulipa kodi. Ufanisi wa ukusanyaji kodi katika nchi ni kipimo kikubwa sana cha umakini na uwajibikaji wa serikali. Kama mnavyojua ukusanyaji mapato unaisaidia serikali kutekeza miradi ya maendeleo ili kupunguza utegemezi kutoka kwa wafadhili.

Mhe. Spika, mswada wa tatu kujadiliwa, ulikuwa ni Mswada wa Kurekebisha Sheria ya Bodi ya Mapato ili Kudhibiti Ukwepaji wa Kodi na Uvujaji wa Mapato ya Serikali. Pamoja na lengo zuri la sheria hii, haitaweza kuleta malengo yaliyokusudiwa iwapo haitasimamiwa na watendaji waadilifu na wenye ujuzi. Kwa mnasaba huo nauomba uongozi wa Bodi ya Mapato kuwapatia watendaji wake mafunzo ya mara kwa mara ili kuwaongezea maarifa na ujuzi katika kazi zao.

Mhe. Spika, mswada wa nne kujadiliwa na Baraza lako ulikuwa ni Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Madawa ya Kulevya na Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Madawa hayo na Kuweka Masharti ya Uzuiaji, Usafirishaji Haramu wa Madawa ya Kulevya. Madhumuni ya mswada huu ni kuzuia usafirishaji haramu wa madawa ya kulevya hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, takriban wajumbe wote waliochangia mswada huu wamezungumza kwa uchungu sana kuhusu tatizo la kusambaa kwa madawa ya kulevya. Baadhi ya wajumbe walipendekeza kuwa wafanyabiashara wa madawa ya kulevya wapewe adhabu ya kifo. Kutolewa kwa pendekezo hili kunaonyesha jinsi Waheshimiwa Wajumbe na wananchi kwa ujumla wanavyokerwa na uhalifu huu.

Mhe. Spika, napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kuwa zipo nchi zenye sheria ya kifo kwa watu wanaobainika kufanya biashara ya madawa ya kulevya, kama vile Singapore na Indonesia. Lakini pamoja na kuwepo kwa hukumu hiyo ya ya kifo, bado tatizo la utumiaji na usafirishaji wa madawa ya kulevya lipo. Madhumuni ya kutoa mfano huu ni kuonyesha kuwa hakuna jibu la mkato katika kukabiliana na uhalifu wa madawa ya kulevya. Kwa mujibu wa Shirika la kutetea haki za Binadamu duniani (*Amnesty International*) hukumu ya kifo haijasaidia sana kupunguza tatizo la utumiaji na usafirishaji wa madawa ya kulevya.

Tatizo la madawa ya kulevya bado ni tishio kubwa kwa nchi nyingi duniani. Licha ya kwamba sheria tuliyoipitisha hapa haitoi adhabu na hukumu ya kifo, mimi ninaamini adhabu ya kifungo cha zaidi ya miaka 30 si ndogo hata kidogo. Hapana shaka tukisimamia vyema sheria hii, itatusaidia sana kupambana na biashara hii ya uhalifu wa madawa ya kulevya. Waheshimiwa Wajumbe

natambua sana na ninakiri kwamba vita dhidi ya madawa ya kulevya ni vita vikali sana. Lakini kama Waswahili Wasemavyo: ”penye nia ipo njia”.

Mhe. Spika, ukiacha bangi takriban madawa yote ya kulevya yanayoingizwa Zanzibar kupitia nchi nyengine na hatimaye kutufikia sisi. Kwa hivyo, suala la ushirikiano na nchi nyengine duniani katika kupambana na madawa ya kulevya ni muhimu sana. Zanzibar itashirikiana na majirani zake katika kupambana na uhalifu huu.

Jambo la pili litakalotusaidia kupambana na madawa ya kulevya ni kuimarisha ulinzi katika mipaka yetu yote. Kwa kuwa Zanzibar ni visiwa, serikali itajitahidi kuweka ulinzi wa kutosha katika bandari zote zilizo rasmi na zisizo rasmi pamoja na viwanja vya ndege.

Mhe. Spika, jambo la tatu linaloweza kutusaidia kupambana na madawa ya kulevya ni kuwa na dhamira ya kisiasa kukabiliana nalo. Nchi zilizopata mafanikio katika vita hivi zimeonyesha dhamira ya kisiasa ya hali ya juu sana katika kuwasaka wahalifu na kuwachukulia hatua kali za kisheria. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kuwa Serikali ya Mapinduzi, inayo dhamira ya kisiasa katika kupambana na usafirishaji wa biashara ya madawa ya kulevya.

Vile vile serikali itaimarisha utendaji wa mahakama. Yamekuwepo malalamiko mengi sana kuhusu uadilifu kwa baadhi ya mahakimu wanaohukumu kesi za madawa ya kulevya. Halikadhalika, serikali itaimarisha utendaji wa Jeshi la Polisi. Biashara ya madawa ya kulevya ina mtandao mpana sana unaowashirikisha matajiri wakubwa. Matajiri hawa katika kuficha uovu wao huwa tayari kutoa rushwa kwa vyombo vya dola. Kwa hivyo, kuna haja ya kuimarisha jeshi letu la polisi, ili askari wake wafanye kazi kwa kuzingatia maadili ya kazi zao.

Mhe. Spika, nimetaja suala hili la uadilifu kwa sababu limekuwa linachukua sehemu kubwa sana katika vita dhidi ya madawa ya kulevya. Tunaweza tukatunga sheria nzuri sana, lakini tukashindwa kuisimamia kutokana na ukosefu wa maadili. Mara nyingi ukosefu wa maadili hutoa mwanya kwa wahalifu kukwepa mkono wa sheria.

Hapa Zanzibar mtakubaliana nami kuwa tunayo mifano hai ya kesi kadhaa zilifutwa au watuhumiwa kuachiwa kwa madai eti ya kukosa ushahidi wa kutosha. Inakuwa vigumu sana kwa mtu mwenye akili timamu kuamini kuwa mtu eti ameze kete 20 au 30 na zitolewe ndani ya tumbo lake, halafu tuambiwe hakuna ushahidi kwa sababu kete zile zilikuwa na saruji. Hapa ama mtu mmoja, amepeleka kete yenye saruji kwa mkemia au mkemia amebadilisha kete za madawa ya kulevya. Huu ni ukosefu wa maadili mema. Tutalisimamia jambo

hili kwa makini ili wakorofi hawa wachache wasipate nafasi ya kubadilisha ushahidi.

Mhe. Spika, mswada wa tano uliojadiliwa na Baraza lako tukufu, ulikuwa ni Mswada wa Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu. Madhumuni ya mswada huu, ni kuzuia usafishaji wa fedha haramu na mapato ya uhalifu. Usafishaji wa fedha haramu ni kitendo cha kuficha fedha zilizopatikana kinyume cha sheria.

Kwa mfano, mtu anayepata fedha kwa kuuza madawa ya kulevya, kufanya ujambazi, wizi au kupokea rushwa, halafu mtu huyo akawekeza fedha hizo katika miradi ya uchumi au katika majengo basi kwa mujibu wa sheria hii atakuwa ametenda kosa la kusafisha madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, wakati wa kujadili mswada huu baadhi ya wajumbe walionyesha wasi wasi wao kuhusu dhamira ya kutungwa mswada huu wa kusafisha fedah haramu. Baadhi ya wajumbe wanadhani kuwa hii ni mbinu na ujanja wa nchi tajiri duniani, kuzuia mitaji mikubwa na fedha kuingia katika nchi maskini.

Mimi kwa mawazo yangu mswada huu naona una maslahi makubwa kwetu zaidi, kuliko nchi zilizoendelea na nchi tajiri kwa ujumla.

Mhe. Spika, sisi sote hapa tunaelewa kuwa vitendo vya kufanya biashara ya madawa ya kulevya, wizi wa fedha na udanganyifu wa kujipatia fedha na mali vinatokea hapa kwetu hivi sasa hata pengine kuliko kwenye nchi tajiri. Usafishaji wa fedha haramu una athari kubwa sana kwetu kiuchumi na kijamii kuliko ilivyo katika nchi tajiri. Zaidi ya hayo uhalifu huu ukiachwa uendelee utasababisha uhalifu mwingine katika jamii utokee kama vile usafirishaji wa madawa ya kulevya. Kwa mnasaba huu Mhe. Spika, sheria hii inakusudia kudhibiti maovu hayo yote.

Mhe. Spika, Baraza lako tukufu lilihitimisha shughuli zake kwa kujadili Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar namba 8 ya 1996 na kanuni zinazoendesha Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena, nachukua fursa hii adhimu, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema ili tuweze kushiriki katika shughuli za mkutano huu. Vile vile niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa kushirikiana na sisi, na kushiriki kikamilifu katika katika mijadala ya hoja mbali mbali zilizowasilishwa katika Baraza lako tukufu. Kwa mnasaba huo basi namuomba Mwenyezi Mungu awajaalie Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu afya njema, kila la kheri na fanaka katika ujenzi wa taifa letu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo basi ninayo heshima kubwa kutamka rasmi kuwa Baraza lako tukufu liahirishwe mpaka tarehe 20/01/2010 saa 3:00 za asubuhi.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.*(Makofi).*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri Kiongozi, kwa hotuba ambayoumetupatia baada ya kumaliza shughuli zetu za Mkutano wa Kumi na Saba.

Waheshimiwa Wajumbe sasa mimi niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri Kiongozi ya kuahirishwa Mkutano huu hadi tarehe 20/01/2010 saa 3:00 za asubuhi barabara wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa).

Waheshimiwa Wajumbe kabla sijaahirisha Mkutano huu, naomba niwakumbushe kwamba kesho ile semina yetu inayohusu afya ya uzazi na uzazi wa mpango itafanyika katika ukumbi wetu huu huu, mnamo saa 2:30 asubuhi kwa ajili ya kujiorodhesha na hatimaye semina yenyewe itaanza rasmi saa 3:00 asubuhi. Tunaombwa sote tuhudhurie semina hiyo.

Pili nichukuwe nafasi hii Waheshimiwa Wajumbe kukushukuruni nyote kwa kunipa mashirikiano makubwa katika kuendesha shughuli zetu za Mkutano huu unaomalizika leo, Mkutano wa Kumi na Saba. Namshukuru Katibu pamoja na watumishi wenzetu anaowaongoza kwa kufanikisha kuwahudumia Waheshimiwa Wajumbe mpaka tukafanya shughuli zetu hizi kwa ufanisi.

Bila ya kuwasahau waandishi wetu wa habari wa vyombo vya serikali, lakini na wa vyombo vya binafsi kwa kushirikiana katika kuendesha shughuli zetu hizi na zikafanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Nakushukuruni kwa kazi nzuri mliyotusaidia kuufanikisha Mkutano huu wa Kumi na Saba.

Waheshimiwa Wajumbe basi baada ya hayo machache naomba sasa niuahirishe Mkutano huu mpaka siku ya Jumatano tarehe 20/01/2010 saa 3:00 barabara za asubuhi. Ahsanteni sana.

(Saa 3:35 asubuhi Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 20/01/2010 saa 3:00 asubuhi)